HOTUBA YA NDUGU GODFREY SABAS NGALEYA KATIBU TAWALA MKOA WA MOROGORO KWENYE SEMINA YA KUTOA ELIMU KWA WALIMU KATIKA KUCHUKUA TAHADHARI DHIDI YA MAFUA MAKALI YA NDEGE NCHINI (AVIAN INFLUENZA) TAREHE 11 NOVEMBA 2008

Ndugu,

Mtaalamu kutoka Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi,

Wataalamu kutoka Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro,

Wataalamu kutoka Halmashauri za Wilaya na Manispaa Morogoro,

Mabibi na Mabwana.

Hii ni mara ya pili kufungua Semina ya aina hii. Mara ya kwanza Semina ni ile ambayo iliwashirikisha wataalamu wa Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam kwa lengo la kuwawezesha kutoa elimu ya tahadhari dhidi ya mafua makali ya ndege kwa wataalamu.

Leo ni zamu yenu kuelimishwa juu ya mafua makali ya ndege ili nanyi mkawafundishe wataalamu katika ngazi ya kata na vijiji ili nao waweze kutoa taarifa sahihi kwa wananchi dhidi ya mafua makali ya ndege. Ni muhimu taarifa zitakazopelekwa kwa wananchi ziwe zinajitosheleza katika hatua za kuufahamu ugonjwa na dalili zake,

kuchukua tahadhari na jinsi ya kukabiliana na ugonjwa endapo kwa bahati mbaya utaingia nchini.

Ndugu Washiriki,
Ugonjwa wa mafua makali ya ndege umeleta hofu miongoni mwa jamii duniani kote na kuufanya kuwa tishio na gumzo kubwa katika jamii. Taarifa za Shirika la Afya kwa Mifugo Duniani (OIE) zinaonyesha kuwa ugonjwa wa mafua makali ya ndege umeenea katika nchi 61 ulimwenguni zikiwemo 11 za Bara la Afrika. Nchi za Afrika zilizothibitishwa kuwa na ugonjwa huu ni Misri, Nigeria, Niger, Burkina Faso, Cameroon, Djibouti, Cote d' Voire, Sudan, Ghana, Togo na Benin. Hali hii inaashiria kuwa ugonjwa huu unaenea kwa kasi kubwa.

Kutokana na ukweli huu, sasa hofu imezikumba nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa huenda ugonjwa huu ukapiga hodi katika nchi hizi wakati wowote na hasa kwa vile tayari umeingia Juba, Kusini mwa Sudan ambayo inapakana na Uganda. Ugonjwa huu unapotokea huleta madhara makubwa kiuchumi, kijamii na kimazingira pia.

Aidha, ugonjwa wa mafua makali ya ndege unaambukiza binadamu kwa hiyo tahadhari zaidi inatakiwa kuchukuliwa

ikiwa ni pamoja na kuweka mikakati ya kuzuia ugonjwa usiingie nchini, na pia endapo kwa bahati mbaya utaingia, basi uweze kudhibitiwa kwa haraka ili usisambae kwenye eneo kubwa. Jukumu kubwa tulilonalo ni la kuwaelimisha wananchi kuhusu madhara ya ugonjwa huo na jinsi ya kuepukana nao.

Ndugu Washiriki,

Njia kuu za kuenea kwa ugonjwa huu ni kupitia ndege pori wanaohama kutoka bara moja hadi jingine na vilevile usafirishaji wa kuku, ndege na mazao yake. Ugonjwa huu umeingia na kuenea bara la Afrika na sehemu nyingine duniani kupitia uingizaji wa kuku, ndege na mazao yake kutoka nchi zilizopatwa na ugonjwa.

Ndugu Washiriki,

Kutokana na tishio la kuingia kwa ugonjwa wa mafua makali ya ndege nchini, Kamati ya Taifa ya Maafa (*Tanzania Disaster Reduction Committee, TANDREC)* katika kikao chake cha tarehe 13/4/2006 iliagiza Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuangalia taratibu zinazotakiwa kufuatwa haraka kukabiliana na tishio la kuingia na kuenea kwa ugonjwa wa

mafua makali ya ndege nchini. Kufikia mwezi Juni, 2006 mpango mkakati ulikuwa umeandaliwa na kusainiwa.

Mpango Mkakati *(Tanzania National Avion Ifluenza Emergence Preparedness & Response Plan)* ulizinduliwa na Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb) Waziri Mkuu tarehe 28 Aprili, 2008 ambapo alieleza kwamba Serikali imeuweka ugonjwa huu kama mojawapo ya majanga ya Taifa. Mkakati huu unatekelezwa na Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara ya Maliasili na Utalii chini ya usimamizi wa Ofisi ya Waziri Mkuu.

Ndugu Washiriki,
Serikali ina jukumu kubwa kimataifa na kitaifa katika kukabiliana na tishio la ugonjwa wa mafua makali ya ndege nchini na inashiriki kikamilifu katika kuchukua tahadhari za kutosha za kuukabili ugonjwa huu.

Kama tusipojiandaa sawasawa, ugonjwa wa mafua makali ya ndege unaweza kuleta athari zifuatazo:

(i) Kuwa kikwazo katika kufikia malengo ya nchi ya kuwa na akiba ya chakula cha kutosha.

(ii) Kuchochea ongezeko la umaskini wa kipato kwa wananchi wengi.
(iii) Kuzorotesha kasi ya wananchi kuendesha shughuli zao za kujikimu.
(iv) Kuathiri pato la fedha za kigeni kutokana na utalii.
(v) Kuongeza gharama za matibabu kwa binadamu na mifugo.

Ndugu Washiriki,
Serikali kwa upande wake imechukua hatua ya kuunda kamati ya kazi na kamati ya wataalamu ambapo kamati zote mbili zinahusisha sekta mbalimbali. Kamati ya Wataalamu ina kamati ndogo kwa ajili ya kuleta ufanisi katika utekelezaji. Dhumuni la kamati ya wataalamu ni kutoa elimu kwa umma kwa njia ya vipindi vya redio, televisheni na vipeperushi ili kuelimisha jamii juu ya dalili na njia za kukabiliana na maambukizo ya ugonjwa wa mafua makali ya ndege.

Hatua nyingine iliyochukuliwa na Serikali ni kujenga uwezo wa kitaaluma, maabara na utafiti juu ya udhibiti wa ugonjwa huu kupitia juhudi za Serikali yenyewe na

miradi ya mashirika ya misaada kutoka Umoja wa Mataifa kwani hili pia ni janga la ulimwengu.

Sababu kubwa ya kuwaweka hapa ni kuwapatia habari na maarifa, kisha muweze kupeleka habari na maarifa hayo kwa wananchi ili ugonjwa huu usiingie nchini. Endapo kwa bahati mbaya ugonjwa utaingia hatuna budi tuwe na uwezo wa kuushambulia mara moja na kuutokomeza ili usijikite nchini.

Ni matarajio yangu kwamba mtakuwa wasikivu, mtajifunza vizuri na kisha kujiandaa kuwapa mafunzo wataalamu katika ngazi ya kata, vijiji, vitongoji na mitaa ili nao waitoe elimu hii kwa wananchi.

Baada ya maelezo hayo, nawatakia ushiriki mzuri na natamka kwamba semina hii imefunguliwa rasmi.

Asanteni kwa kunisikiliza.